TANGAZO LA SERIKALI NA. 542 la tarehe 5/7/2024

SHERIA YA MISITU
(SURA YA 323)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 22(1))*

AMRI YA KUTANGAZA MSITU WA HIFADHI MLUNGUI YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Msitu wa Hifadhi Mlungui ya Mwaka 2024.

Tangazo

2. Eneo la ardhi ya mataji wazi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi Mlungui.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA MUHEZA

MSITU WA HIFADHI MLUNGUI

*Makadirio ya Eneo:* Hekta 200 au Kilometa za Mraba 0.2

Unakopatikana na Mipaka

Eneo lote la ardhi ya mataji wazi awali chini ya Msitu wa Mlungui linalopatikana Wilaya ya Muheza, Mkoa wa Tanga kama lilivyochorwa katika Ramani ya Idara ya Upimaji Jb 2247 ya mwaka 1994 (Skeli 1:5,000) iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na lenye mipaka ifuatayo:

*Tangazo La Serikali Na. 542 (Linaendelea)*




Dodoma, ANGELLAH JASMINE KAIRUKI

__24 Mei, 2024 *Waziri wa Maliasili na Utalii*